TANGAZO LA SERIKALI NA. 550 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA UFUGAJI NYUKI
(SURA YA 224)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 11(1))*

AMRI YA KUTANGAZA HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA KWENYUNGA – MAGIRI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Hifadhi ya Nyuki ya Taifa Kwenyunga- Magiri ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyuki Kwenyunga-Magiri.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA HANDENI

HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA KWENYUNGA- MAGIRI

*Makadirio ya eneo*: Hekta 129.35 au Kilometa za Mraba 1.29

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Kwenyunga-Magiri linalopatikana Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2778 ya mwaka 2018 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 550 (Linaendelea)*




Dodoma, ANGELLAH JASMINE KAIRUKI

___24 Mei, 2024 *Waziri wa Maliasili na Utalii*